وَصِيَّةٌ مِنَ العُلَمَاءِ

WASIA KUTOKA KWA MALLAMAA

Ametaja Ibn Abi Shaiba kwa sanadi, kutoka kwa Abu 'Aun رَحِمَهُمَا اللهُ amesema:

"كَانَ أَهْلُ الْخَيْرِ إِذَا الْتَقَوْا يُوصِي بَعْضُهُمْ بَعْضًا بِثَلَاثٍ، وَإِذَا غَابُوا كَتَبَ بَعْضُهُمْ إِلَى بَعْضٍ «مَنْ عَمِلَ لِآخِرَتِهِ كَفَاهُ اللَّهُ دُنْيَاهُ، وَمَنْ أَصْلَحَ فِيمَا بَيْنَهُ وَبَيْنَ اللَّهِ كَفَاهُ اللَّهُ النَّاسَ، وَمَنْ أَصْلَحَ سَرِيرَتَهُ أَصْلَحَ اللَّهُ عَلَانِيَتَهُ»

[Walikuwa watu wema pindi wakikutana, wananasihiana wao kwa wao kwa mambo matatu, na ikiwa hawapo 'karibu' mmoja wao anamuandikia mwingine "Mwenye kufanya amali kwa ajili ya akhera yake, Allaah humtosheleza katika (maisha yake) ya dunia. Na anayetengeza yaliyo baina yake na baina ya Allaah, basi Allaah atamtosheleza na (kuwahitajia) watu. Na atakayetengeneza Usiri/Undani wake, basi Allaah atamtengenezea dhahiri yake"]. Muswannaf Ibn Abi Shaiba (34988)

Mwandishi

Sheikh Ahmad Al-Mazrui

Mfasiri

Abu Halima Arafat

بسم الله الرحمن الرحيم

Ufafanuzi: Haya ni maneno yenye manufaa ambayo yamekusanya mambo matatu muhimu:

Jambo la Kwanza: ni mtu kutengeneza usiri wake, nako ni kuwa mnyenyekevu, mwenye khofu, na awe ni mwenye kufanya ibada kwa kutarajia thawabu na khofu ya kuogopa adhabu ya Allaah Mtukufu, pamoja na kuufungamanisha moyo wake na Allaah kila wakati, mtu yeyote ambaye atakuwa katika hali hii, Allaah atamtengenezea dhahiri yake; mwili wake, usikivu wake (kusikiliza), uoni wake (kuona kwake), kutembea, kuzungumza kwake, n.k. asili ya mtu kuwa nzuri dhahiri yake ni kwa sababu ya kutengenezeka moyo wake, ama mtu kuonyesha umaridadi wa dhahiri, (usafi wa mwili, mavazi n.k) bila kupatiliza moyo wake, hiyo ni sababu ya kuharibika moyo wake, (kwa kuacha kutengeneza mahusiano mazuri baina yako na Mola wako mlezi).

Amesema Mtume **-Swalla Llaahu alaihi Wasallam-:**

«أَلَا وَإِنَّ فِي الْجَسَدِ مُضْغَةً إِذَا صَلَحَتْ صَلَحَ الْجَسَدُ كُلُّهُ، وَإِذَا فَسَدَتْ فَسَدَ الْجَسَدُ كُلُّهُ، أَلَا وَهِيَ الْقَلْبُ»

"Zindukeni, hakika katika kiwiliwili kuna kipande cha nyama, kikitengenea (kikiwa kizuri kipande hicho) basi umetengenea mwili wote, zindukeni (jueni) kuwa kipande hicho ni moyo"[1].

Jambo la Pili: Mwenye kutengeneza mahusiano mazuri baina yake na Mola wake, Allaah huyapatanisha yaliyo baina yake na watu, (maana yake ni kwamba): mwenye kutengeneza yaliyo baina yake na Mola wake, kwa kumuamini Allaah, kutenda amali njema, na kuithibitisha Itikadi sahihi (ya Ahlus Sunnah wal-Jamaa), kusimamisha swala, kufanya aliyoamrisha na kuacha aliyokataza, Allaah atayapatanisha yaliyo baina yake na watu; kwa

[1]- Bukhari (52).

sababu mwenye kutengeneza mahusiano mazuri na Allaah, Allaah anampenda, na huwafanya watu wampende mtu huyo.

Amesema Allaah Ta'alaa:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ سَيَجۡعَلُ لَهُمُ ٱلرَّحۡمَٰنُ وُدّٗا﴾

"Hakika wale walioamini na wakatenda mema Allaah mwingi wa rehma atawajaalia mapenzi"[2].

Allaah anawapenda na anawafanya waja wake waumini wawapende watu hao[3], na imekuja katika hadithi:

«إِذَا أَحَبَّ اللَّهُ العَبْدَ نَادَى جِبْرِيلَ: إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ فُلاَنًا فَأَحْبِبْهُ، فَيُحِبُّهُ جِبْرِيلُ، فَيُنَادِي جِبْرِيلُ فِي أَهْلِ السَّمَاءِ: إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ فُلاَنًا فَأَحِبُّوهُ، فَيُحِبُّهُ أَهْلُ السَّمَاءِ، ثُمَّ يُوضَعُ لَهُ القَبُولُ فِي الأَرْضِ»

"Allaah akimpenda mja anamwita Jibril (anamwambia): Hakika Allaah anampenda mtu fulani, basi mpende, kisha Jibril anampenda, na (Jibril) anawaita viumbe walio mbinguni (anawaambia): Hakika Allaah anampenda mtu fulani, basi (na nyinyi) mpendeni, kisha viumbe wa mbinguni wanampenda (mtu huyo), kisha anawekewa yeye qabuli (kukubalika) duniani"[4] [5].

Jambo la Tatu: Mwenye kujishughulisha na akhera yake Allaah humtosheleza yeye kwa riziki yake hapa duniani, imekuja katika hadithi:

«وَمَنْ كَانَتْ الْآخِرَةُ نِيَّتَهُ جَمَعَ اللَّهُ لَهُ أَمْرَهُ، وَجَعَلَ غِنَاهُ فِي قَلْبِهِ، وَأَتَتْهُ الدُّنْيَا وَهِيَ رَاغِمَةٌ»

"Na yule ambaye itakuwa akhera ndio kusudio lake, Allaah atamkusanyia yeye jambo lake (atampatia dunia na akhera), na atajaalia kutosheka kwake ndani ya moyo wake, na itamjilia yeye dunia hali ya kuwa inanyenyekea"[6].

2- Surat Maryam/96.

3-Amesema Imamu Al-Baghwiy -Allaah amrehemu-: **[Amesema Mujahid: Allaah anawapenda, na anawafanya wapendwe na waja wake wauimini]**.

4- Bukhari (3209).

5- Allaah huweka mapenzi kwa Waislamu, humpenda na kumtaja kwa kheri hata baada ya kufa.

6- Sunan Ibn Maajah (4105).

Yule mwenye kuishughulikia akhera yake itamjia yeye dunia hali ya kuwa inanyenyekea, na Allaah atamfanyia yeye wepesi katika kazi zake za utafutaji wa riziki. Na yule mwenye kuitanguliza zaidi dunia yake na akaipuuza akhera yake, hakika mtu huyu ameipoteza dunia pamoja na akhera yake, kama ilivyokuja katika hadithi:

«مَنْ كَانَتِ الدُّنْيَا هَمَّهُ، فَرَّقَ اللَّهُ عَلَيْهِ أَمْرَهُ، وَجَعَلَ فَقْرَهُ بَيْنَ عَيْنَيْهِ، وَلَمْ يَأْتِهِ مِنَ الدُّنْيَا إِلَّا مَا كُتِبَ لَهُ»

"Yule ambaye itakuwa dunia ndio tamaa (malengo) yake, Allaah atamvurugia yeye jambo lake, na atajaalia umasikini wake mbele ya macho yake, na hakitamjia yeye katika dunia yake isipokuwa kile alichoandikiwa"[7].

Haiwezekani katika moyo wa mtu kukusanyika mapenzi ya dunia na akhera wakati mmoja, lazima kimoja kitadhurika, lakini jambo kubwa kwa mja ni kutanguliza akhera yake, kwa sababu ndio yenye kubaki milele, na dunia na vilivyomo ni vyenye kumalizika na kutoweka. Pia utulivu wa moyo wa mtu upo katika kujikurubisha na Mola wake mlezi, kupitia mafunzo sahihi ya Mtume **– Swalla Llaahu alaihi wasallam –.**

Ewe Allaah turuzuku mapenzi ya kukupenda wewe na Mtume wako **– Swalla Llaahu alaihi wasallam –** na kupenda kutenda amali njema zenye kutukurubisha kwako.

Markaz Sheikhil Islaam Ibn Taymiyyah,

29/5/1444H – 22/12/2022M,

Pongwe Tanga,

Tanzania.

[7]- Sunan Ibn Maajah (4105).